

UUNGU

Nini Hasa Maana ya Kibiblia ya Maneno ya Baba: "Mimi Leo Nimekuzaa"?

Biblia inatoa rejea kadhaa zinazoonyesha matukio kadhaa ya kuzaliwa kwa Yesu. Pia kuna wakati inarejea mazungumzo yaliyofanyika kati ya Mungu Baba na Yesu, ambayo...

PR. ALMODAD AMOS YARAGWILLER 2026

YouTube: Maswali na Majibu Ep 01. Maana ya Mimi Leo Nimekuzaa | Pr. Almodad Amos #mahubiri #imaniyakweli

Utangulizi

Biblia inatoa rejea kadhaa zinazoonyesha matukio kadhaa ya kuzaliwa kwa Yesu. Pia kuna wakati inarejea mazungumzo yaliyofanyika kati ya Mungu Baba na Yesu, ambayo yanaonyesha Yesu alizaliwa na Baba. Wengi wameyachukua maandiko hayo bila kuyachunguza na wakahitimisha kuwa: kwanza, kuna wakati Yesu hakuwepo, bali Mungu Baba alikuwepo kwanza na hivyo uhai wa Yesu unatokana na tendo la Baba kumzaa Mwana kama Biblia inavyoeleza; Pili, wapo waliofikia hitimisho kuwa kwa maelezo hayo ya Kibiblia, Biblia haifai tena kuaminika maana inawezekana je, Mungu azae na hali Yeye si kiumbe na hana mke?

Itakushangaza kugundua kuwa habari ya kuzaliwa kwa Yesu katika muktadha wa Baba kumzaa Yesu, haimaanishi hata kidogo habari ya mianzo ya uhai wa Yesu wala haiongelei au kuhusiana hata kidogo na habari ya uzazi wa kimwili kama tunaoushuhudia kwa wanadamu au wanyama. Nini maana ya maneno hayo nimekuzaa?

Matumizi ya Lugha ya Picha

Ni muhimu tunapoisoma Biblia tuiache yenyewe ijifafanue maana inauwezo wa kujifafanua yenyewe. Wakati mwingine unapoisoma Biblia usipochunguza kwa umakini linaloongelewa unaweza kuondoka na maana yako Binafsi iliyopotoka na ukadhani uko salama, lakini ukweli ni kwamba baadhi ya maandiko ni mafumbo, mifano, na vielelelezo na

hayakukusudiwa kuchukuliwa moja kwa moja kama yalivyo, bali ilikusudiwa msomaji achunguze maana asilia iliyokusudiwa na mwandishi.

Wajibu wetu hapa ni kutafuta kuelewa kile mwandishi alichokusudia alipozungumzia habari za Yesu kuzaliwa. Sisi hatupaswi kuzipatia maana aya tunazozisoma, inafaa aya zenyewe zijieleze kwamba zinataka sisi tuelewe nini. Sasa hebu tuchunguze nini Biblia inamaanisha inapozungumzia habari ya kuzaliwa.

Maana Nne za Kuzaliwa katika Biblia

Neno kuzaliwa katika Biblia halibebi maana moja tu peke yake. Linaweza kuwa na maana takribani nne kama ifuatavyo:

Maana ya 01: Tendo la mtu kutoka tumboni mwa mama yake

> Akapata mimba tena, akazaa mwana, akamwita jina lake Onani.
>
> **MWANZO 38:4 SUV**

Katika muktadha wa aya hii neno kuzaliwa linamaanisha kitendo cha kutoka kwa mtoto kutoka mwilini mwa mama yake; mwanzo wa maisha ya kiumbe kitakachojitegemea kimwili.

Je, Yesu alizaliwa aina hii ya Uzazi? Majibu ni ndiyo:

> maana leo katika mji wa Daudi amezaliwa, kwa ajili yenu, Mwokozi, ndiye Kristo Bwana.
>
> **LUKA 2:11 SUV**

Maana hii ya kwanza inayoongelewa hapa haina mgogoro wowote maana iko wazi kabisa kwamba inazungumzia tukio la kuzaliwa kwa Yesu na mwanamke aliyeitwa Mariamu. Ni muhimu kujua kuwa hii haikua mwanzo wa maisha ya Yesu katika umilele, isipokua ilikua mwanzo wa maisha ya Yesu alipoutwaa mwili wa Binadamu hapa duniani kama anavyosema Paulo:

> ambaye yeye mwanzo alikuwa yuna namna ya Mungu, naye hakuona kule kuwa sawa na Mungu kuwa ni kitu cha kushikamana nacho; bali alijifanya kuwa hana utukufu, akatwaa namna ya mtumwa, akawa ana mfano wa wanadamu;
>
> **WAFILIPI 2:6-7 SUV**

Maana ya 02: Ubatizo

Maana ya pili ya neno kuzaliwa katika Biblia ni tendo la mtu kubatizwa. Katika Biblia, ubatizo unaonekana kama ishara ya kuzaliwa mara ya pili, ukionyesha kuzaliwa upya kiroho. Kupitia ubatizo, mtu hutangaza hadharani imani yake kwa Yesu Kristo na kujitoa kwake kikamilifu kwa maisha mapya ndani Yake. Kitendo hiki ambacho humaanisha kusafishwa kwa dhambi na mianzo mipya ya safari ya maisha ya Imani, kinafananishwa na mianzo mipya ya maisha ya kiumbe kinapozaliwa; katika maandiko tendo hili linaitwa Kuzaliwa.

Mfano unaojulikana sana kuhusiana na hili ni ule uliopo katika mazungumzo ya Yesu alipokuwa akizungumza na Nikodemo:

> Yesu akajibu, akamwambia, Amin, amin, nakuambia, Mtu asipozaliwa mara ya pili, hawezi kuuona ufalme wa Mungu. Nikodemo akamwambia, Awezaje mtu kuzaliwa, akiwa mzee? Aweza kuingia tumboni mwa mamaye mara ya pili akazaliwa? Yesu akajibu, Amin, amin, nakuambia, Mtu asipozaliwa kwa maji na kwa Roho, hawezi kuuingia ufalme wa Mungu.
>
> **YOHANA 3:3-5 SUV**

Maana ya 03: Utakaso unafanywa na Roho Mtakatifu

Maana ya tatu ya neno Kuzaliwa inapatikana katika Tito 3:5. Hii ni tendo la mtu kupewa uwezo wa kuondokana na maovu aliyokua akiyafanya huko nyuma ili aweze kuishi maisha matakatifu. Ni kitendo cha kuanza maisha mapya ya utakatifu kwa mara nyingine tena, ambapo mtu anawezeshwa kulifanya hilo kwa uwezo wa Roho Mtakatifu. Wakati ubatizo unapofanyika, mambo mawili yanafanyika, kuna tendo la mtu kubatizwa, ambalo ni tendo la imani linaloonekana kwa nje, kama tulivyoeleza katika hatua iliyopita, na kisha kuna badiliko la ndani ya moyo ambalo hilo halifanywi na mtu bali linafanywa na Mungu mwenyewe. Hilo tendo linaitwa kuoshwa kwa kuzaliwa upya. Andiko linasema:

> Maana hapo zamani sisi nasi tulikuwa hatuna akili, tulikuwa waasi, tumedanganywa, huku tukitumikia tamaa na anasa za namna nyingi, tukiishi katika uovu na husuda, tukichukiza na kuchukiana. Lakini wema wake Mwokozi wetu Mungu, na upendo wake kwa wanadamu, ulipofunuliwa, alituokoa; si kwa sababu ya matendo ya haki tuliyoyatenda sisi; bali kwa rehema yake, kwa kuoshwa kwa kuzaliwa kwa pili na kufanywa upya na Roho Mtakatifu;
>
> **TITO 3:3-5 SUV**

Hili tendo la kuzaliwa kwa Pili kwa maana iliyoelezwa katika kipengele hiki kwa Kiyunani (ambayo ni lugha iliyotumika kuandika aya ya Tito 3:5) linaitwa “loutron” (pia lipo ktk Waefeso 5:26), yaani, “kuoshwa” kiroho, ambako kunamtakasa mwanadamu kutokana na mwelekeo mbaya ulioelezewa katika Tito 3:3.[1] Neno hili linatumika pia katika Waefeso 5:26 na safari hii tafsiri yake kwa lugha ya kiswahili ni neno takasa:

> ili makusudi alitakase na kulisafisha kwa maji katika neno;
>
> **WAEFESO 5:26 SUV**

[1] *Francis D. Nichol, ed., The Seventh-Day Adventist Bible Commentary, vol. 7 (Review and Herald Publishing Association, 1980), 370.*

Maana ya 04: Ufufuo wa Yesu Kristo Kutoka Kaburini

Biblia inaeleza waziwazi kabisa kwamba Mungu Baba alimzaa Yesu Kristo. Jambo hili linawakera sana hasa ndugu zetu Waislam ambao wanaona kama ni kichekesho kusema kwamba Mungu alizaa. Sasa wanauliza alizaa na nani? Na huyo Mariam ambaye Yesu alizaliwa kwake katika hali hiyo alikua mwanamke wa aina gani? Hebu kwanza tutazame aya zinazoonyesha kuwa Baba alimzaa Yesu:

> Nitaihubiri amri; BWANA aliniambia, Ndiwe mwanangu, Mimi leo nimekuzaa.
>
> **ZABURI 2:7 SUV**

> Kwa maana alimwambia malaika yupi wakati wo wote, Ndiwe mwanangu, Mimi leo nimekuzaa? Na tena Mimi nitakuwa kwake baba, Na yeye atakuwa kwangu mwana?
>
> **WAEBRANIA 1:5 SUV**

> Vivyo hivyo Kristo naye hakujitukuza nafsi yake kufanywa kuhani mkuu, lakini yeye aliyemwambia, Ndiwe mwanangu, Mimi leo nimekuzaa.
>
> **WAEBRANIA 5:5 SUV**

Yesu mwenyewe pia anazungumza katika Mithali kwamba alizaliwa kabla milima na vilima havijakuwepo:

> BWANA alikuwa nami katika mwanzo wa njia yake, Kabla ya matendo yake ya kale. Nalitukuka tokea milele, tangu awali, Kabla haijawako dunia. Wakati visipokuwako vilindi nalizaliwa, Wakati zisipokuwako chemchemi zilizojaa maji. Kabla milima haijawekwa imara, Kabla ya vilima nalizaliwa.
>
> **MITHALI 8:22–25 SUV**

Bila shaka huu uzao anaoungelea Yesu, si ule wa kuzaliwa na Mariam, kwa sababu wakati huu unaozungumzwa katika Mithali, Mariam alikua bado hajazaliwa. Kwa hiyo tunaona kuwa Yesu alizaliwa kabla ya dunia kuumbwa, lakini pia alizaliwa baada ya dunia kuumbwa na Mariam. La

msingi kuelewa hapa ni kwamba maana ya neno kuzaliwa inayozungumziwa katika Kitabu cha Zaburi 2:7, Waebrania 1:5, Waebrania 5:5 na Mithali 8:22-25 haikua inaongelea habari za kuanza kwa maisha ya Kristo.

Lugha inayotumika hapo ni lugha ya Kiunabii ambayo mara nyingi inatumia mafumbo katika kuwasilisha ujumbe wake uliokusudiwa. Ikiwa Biblia yenyewe, bila kusaidiwa na mawazo ya watu binafsi au vyanzo vya nje, isingefafanua zaidi kuhusu maana ya tendo la Baba kumzaa Yesu, basi tungekua na haki mbili za msingi. Kwanza, tungekua na haki ya kusema kuwa Yesu mtoto tu kwa Baba kama sisi tulivyo watoto kwa Baba yetu wa Mbinguni, na haki ya pili ambayo tungekuwa nayo, ingekua kuikataa Biblia na kuihesabu kuwa si chanzo cha kuaminika. Lakini sasa Biblia haikuishia hapo, inafafanua zaidi kuhusu habari ya Baba kumzaa Yesu, na inaeleza kuwa tendo hilo halifanani wala halikaribiani hata kidogo na uzazi ambao wanadamu au wanyama au viumbe vingine huwa vinalifanya (yaani kuanza kwa maisha ya nafsi ikitoka ndani ya au katika nafsi nyingine). Hebu tazama Biblia inavyofafanua jambo hili:

> ya kwamba Mungu amewatimizia watoto wetu **ahadi hiyo**, **kwa kumfufua Yesu**; kama ilivyoandikwa katika Zaburi ya pili, Wewe ndiwe Mwanangu, mimi leo nimekuzaa.
>
> **MATENDO 13:33 (SUV)**

Aya iko wazi kabisa wala haina kona-kona, inaeleza kuwa suala la Baba kumwambia Yesu leo mimi nimekuzaa, ni suala ambalo moja kwa moja lilikua linaongelea habari ya ufufuo wa Yesu.

Hii inatuondolea utata kuhusu Yesu alizaliwa mara ngapi? Inaondoa utata kuhusu huyo Mariamu mama yake Yesu, kwamba sasa atakuwa na waume wangapi na atakua yuko je, hasa? Inaondoa utata kuhusu nafasi ya Yesu kimahusiano na Mungu Baba na inatukumbusha tu kuwa hakuna wakati ambao Yesu hakuwepo maana hilo suala la Baba kumwambia leo nimekuzaa, kumbe ilikuwa ni mazungumzo na ahadi ambayo Mungu alikua anamwambia Yesu, ulikua ni utabiri ambao Mungu mwenyewe aliutoa ya kwamba huko mbeleni nitakufufua kutoka katika wafu; na siku Yesu alipofufuka andiko katika matendo ya Mitume linasema, ahadi hiyo ya Yesu kuzaliwa na Baba ilitimia. Hebu soma tena aya hizi kwa kutafakari kwa mara nyingine tena:

> Nitaihubiri amri; BWANA aliniambia, Ndiwe mwanangu, Mimi leo nimekuzaa.
>
> **ZABURI 2:7 (SUV)**

> ya kwamba Mungu amewatimizia watoto wetu **ahadi hiyo**, **kwa kumfufua Yesu**; kama ilivyoandikwa katika Zaburi ya pili, Wewe ndiwe Mwanangu, mimi leo nimekuzaa.
>
> **MATENDO 13:33 (SUV)**

Zaidi kutoka Injili Milele

Makala, vitabu, video na sauti zaidi zinapatikana kwenye maktaba ya Injili Milele:

Je, Sabato Ilikoma kwa Kuwa Ilikuwa Kivuli cha Mambo Yajayo?
Sabato · PDF

Sanduku la Agano: Je, Litaonekana Tena?
Unabii · PDF

Je, Yesu ni “Mungu Mwana” au “Mwana wa Mungu”?
Uungu · Video

Kwa Nini Mungu Alimuumba Lusifa?
Pambano Kuu · PDF

Papa Gregory XIII Alipobadilisha Kalenda: Siku Zilivurugwa, Sabato Ilipotea?
Sabato · PDF

Je, ni Lazima Kupiga Magoti Wakati wa Maombi?
Ibada · PDF

Injili Milele

almodad-2.github.io/injili-milele/sw/

WhatsApp +255 718 834 621 · modaofhope@gmail.com

© 2026 Pr. Almodad Amos Yaragwiller · Injili Milele. Haki zote zimehifadhiwa. Usiuze nakala hii bila ruhusa ya maandishi ya mwandishi.